

# Mtie Kamba Mumeo

## Khadija Kopa

Kama unaweza mtie kamba mumeo umzuie  
Ukitahamaki chini ka chimba mumeo ninae mie\*2  
Chini ka chimba ninae mie\*2  
Ninae mie ninae mie.\*2  
Chini ka chimba ninae mie  
Ninae mie natamba nae.

### Verse1

Mbio mbio kanikimbilia(mumeweo)  
Akaniomba mapenzi\*2  
Namii nami nikamringia  
Nikaona nikaona hayawezi.\*2  
Kumbe kumbe amenikamia  
Kanizingua kanizingua kichizi  
Nami nikamridhia\*2  
Kila kitu LA azizi  
Nikamwambia chukua upendacho LA azizi...

### (Chorus)

### Verse 2

Kwa yangu makashkashi  
Aliingia uchizi.\*2  
Alihamisha mataki  
Alipojaa njozi\*2  
Nikampa nikampa mishkaki.  
Na chai ya tangawizi\*2  
Aliniambia sichoki(mie)  
Siogopi fumanizi\*2

### (Chorus)

### Verse 3

Bwana huyu bwana huyu kaniganda mie  
Wala hanipi pumzi\*2  
Namimi namimi ninayapenda  
Nazidi kukaza uzi\*2

We baki baki unavyokarega  
Hakupendi hakupendi hujijuzi\*2  
Wala hujui kupendaaa  
Na mabao huyamalizi.\*2

(Chorus)

Lyrics Submitted by Khadija

Lyrics provided by  
<https://damnlyrics.com/>